

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
IDARA YA HABARI-MAELEZO

Simu: +255-22-2126826,  
Baruapepe: [maelezo@habari.go.tz](mailto:maelezo@habari.go.tz),  
Tovuti: [www.tanzania.go.tz](http://www.tanzania.go.tz),  
Faksi: +255-22-2126834.



Ghorofa ya 3, JNICC,  
S.L.P 8031,  
DAR ES SALAAM.

## TAARIFA KWA UMMA

### SERIKALI YAKANUSHA TAARIFA ILIYOSAMBAZWA KUPITIA CCTV-AFRIKA

Dar es Salaam, Januari 21, 2019:

Kwa siku kadhaa sasa kumekuwa na taarifa inayosambaa kwa njia ya video ambayo baada ya uchunguzi wetu tumebaini ilirushwa mwaka 2016 na Kituo cha Televisheni cha China (CCTV-Afrika), ikielezea hisia za uwepo wa viashiria vya kundi la Al-Shaabab nchini Tanzania.

Msingi wa taarifa hiyo ya mwaka 2016 ni ripoti yenyewe kurasa 53 iliyoandaliwa na wataalamu wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Mashariki mwa Afrika (IGAD), ambayo hata hivyo haikujikita kwenye utafiti wowote wa moja kwa moja kuhusu Tanzania bali hisia za watu na makundi mbalimbali katika nchi za Kenya, Ethiopia na Somalia.

Tumewasiliana na wamiliki wa *CCTV-Afrika* na wamekiri kuwa taarifa hiyo haikuwa na ushahidi wa maana na kwamba sio wao waliosambaza tena video hiyo, ikionekana dhahiri kuwa kuna watu wenye nia mbaya na nchi yetu wameitumia video hiyo ya mwaka 2016 kwa malengo hasi dhidi ya Tanzania.

Kwa taarifa hii, pamoja na hatua nyingine ambazo Serikali na *CCTV* yenyewe tunazichukua, umma unaarifiwa kuzipuuza taarifa zozote zinazoipaka matope Tanzania na kuihusisha na kundi lolote la kigaidi. *CCTV* wameshafanya uamuzi wa kuifuta video hiyo katika mitandao yao.

Napenda kuuhakikishia umma na watu wengine wote wenye mapenzi mema na Tanzania kuwa nchi yetu iko salama, na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama viko makini kufuatilia na kuchukua hatua iwapo kuna viashiria vyovyyote vya kuharibu wa amani popote nchini.

Kwa taarifa hii katika lugha ya Kiingereza fungua Kituo cha Habari/Media Center/taarifa kwa umma/press releases katika [www.maelezo.go.tz](http://www.maelezo.go.tz).

Imetolewa na:

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Hassan Abbasi'.

**Dkt. Hassan Abbasi**

**Mkurugenzi, Idara ya Habari-MAELEZO na Msemaji Mkuu wa Serikali.**

